SHULE YA SEKONDARI CHABUTWA
S.L.P 121,
SIKONGE – TABORA
Barua pepe: chabutwasekondari@gmail.com
Mobile: 0676-407088 / 0683-503200
Tarehe: ....../....../........

Kumb Na. ..........................................................
Jina la mwanafunzi. ................................................
S.L.P ...................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHABUTWA ILIYOPO WILAYA YA SIKONGE, MKOA WA TABORA MWAKA...........**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **CHABUTWA** mwaka ...........Shule ya sekondari chabutwa ipo umbali wa km 10 kusini mwa Halmashauri ya wilaya ya Sikonge.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ............ na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe .../..../........ na mwisho wa kuripoti ni tarehe .../....../........ ndani ya siku saba (7)

**2. MAMBO MUHIMU KWA WANAOJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHABUTWA**

**A. WASICHANA**

i. Sketi mbili (2) za rangi ya ugoro ndefu zinazofika kwenye kifundo cha kisigino cha mguu zenye marinda ya wastani. Fika shuleni upate maelekezo zaidi kwa makamu mkuu wa shule.
ii. Blauzi (shati) mbili nyeupe za kitambaa cha tetron zenye mikono mifupi na zisizo na urembo.
iii. Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi (visivyogonga) na visiwe vibajaji au yeboyebo.
iv. Soksi nyeupe.
v. Kwa waislamu vazi la hijabu linaruhusiwa- kitambaa cha kichwani (Head square) cheupe cha tetron kisicho na wa aina yoyote.
vi. Nguo za michezo, Sketi mbili zisizo bana za rango nyeusi na T-shirt mbili za mikono mifupi za rangi ya njano na zenye nembo ya shule inapatikana hapa hapa shuleni CHABUTWA SEKONDARI.

**B. WAVULANA**

i. Suruali mbili za rangi ya ugoro (siyo dengizi au jinsi)
ii. Shati mbili nyeupe (tetroni) za mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye kamba (visivyogonga)

iv. Mkanda mweusi.
v. Nguo za michezo –bukta zisizobana za rangi ya bluu na T-sheti mbili (2) za mikono mifupi rangi ya njano yenye nembo ya shule inapatikana hapa CHABUTWA SEKONDARI.

2.2 .Daftari kumi na moja (11) ,kalamu na mkebe wa hesabu.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dahamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi ,wazazi ,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinagana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote .
i) Kutunza mali za umma.

## 3.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi ,cocaine,mirungi.kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa mmakusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa .
j) Kutoa mimba.

K. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l. Kukataa adhabu kwa makusudi.

m. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo riporti shuleni.
b. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c. Fomu ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa umakini maelekezo/maagizo haya na kutekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

THE HEADMISTRESS
CHABUTWA SEC. SCHOO.
P. O. BOX 121 SIKONGE

...............Mtro...............

**M.P MAYUNGA**

**MKUU WA SHULE**

## MINISTRY OF EDUCATION ,SCIENCE AND TECHNOLOGY

## CHABUTWA SECONDARY SCHOOL

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government medical officer and returned to the Headmistress, Chabutwa secondary school, P.O.BOX 121 SIKONGE)

Name.......................................................................................................

Please examine the student named above and comment on his /her health by recording to the following items. Kindly put a tick infront cf either YES or NO whichever is applicable.

1. Does the student have problem in connection with:

A. Sight........................................................................ 1.NO
   IF YES state.............................................................. 2. YES

B. Hearing .................................................................... 1. NO
   IF YES state.............................................................. 2.YES

C. T.B .......................................................................... 1.NO
   IF YES state.............................................................. 2.YES

D. Blood Pressure.......................................................... 1.NO
   IF YES state.............................................................. 2.YES

E. Asthma..................................................................... 1.NO
   IF YES state.............................................................. 2.YES

F. Any other Health problems........................................ 1.NO
   IF YES state.............................................................. 2.YES

Do you therefore recorded said student medically fit for studentship at this school IF NO.Please state .............................................................. 1.NO
2.YES

Name and signature................................................ Designation..........................

Date............................................. Official Stamp..............................

# SHULE YA SEKONDARI CHABUTWA

## FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE KWA MZAZI NA MWANAFUNZI

### I. KUJIANDIKISHA

(Ijazwe na kukabidhiwa kwa ofisi ya kujiandikisha shule)

1) Jina kamili la Mwanafunzi ..............................................................................
2) Tarehe ya Kuzaliwa ..........................................................................................
3) Mahali alipozaliwa (Wilaya) ..............................................................................
4) Uraia ............................................
5) Shule ya Msingi anapotoka ...................................................
6) Dini ......................................................................
7) Mahali anapoishi sasa kwa mwanafunzi wasiolala bweni ....................................

### II. ENEO ANALOISHI

1) Wilaya .......................................

2) Tarafa .......................................

3) Kijiji ...........................................

4) Mtaa/Kitongoji ..........................

### III. MZAZI NA NDUGU WA KARIBU

1) Jina la mzazi/Mlezi ..................................taja ndugu wengine wa karibu

a) ..........................................................

b) ..........................................................

c) ..........................................................

2) Kazi ya Mzazi/mlezi .....................................

3) Anuani ya Mzazi/Mlezi ................................................ Simu .......................

### IV) AHADI YA MWANAFUNZI:

Mimi .................................................................nakubali nafasi hii niliyopewa na ninaahidi kutii kikamilifu sheria, kanuni na taratibu zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa shule ya sekondari Chabutwa.

Sahihi ya Mwanafunzi: ...............................

Sahihi ya Mzazi au Mlezi: ..........................

Tarehe: .....................................